**EPISODE 7 “VIRUS, SPAM AND MUSIC PIRATES”**

| | |
|---|---|
| **SCRIPT WRITER** | **Njoki Muhoho** |
| **EDITOR** | **Jan-Philipp Scholz** |
| **KISUAHELI:** | **Eric Ponda** |

**CHARACTERS**

| | |
|---|---|
| **ANNOUNCER** | Male Adult |
| **ZAPCOM** | A 23-year-old computer geek, by village standards. |
| **GEORGE** | 20 years old. Waits tables at his Uncle Kilu’s restaurant. |
| **UNCLE KILU** | 55 years old. George’s uncle, owner of KULA TU FOODS. |
| **OMWA** | 19 years old and jobless. Female. |

**INTRO**

1. **MUSIC: THEME MUSIC**

*2.* **ANNOUNCER** NI WAKATI MWENGINE MASIKILIZAJI WA DEUTSCHE WELLE TUNAPOUNGANA NAWE MAHALI POPOTE ULIPO KUKULETEA MAKALA NYINGINE YA MFULULIZO WA VIPINDI VYA LEARNING BY EAR NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO. NI MAKALA YA 7 YA MCHEZO HUU WA REDIO KUHUSU

TEKNOLOJIA MPYA YA HABARI NA MAWASILIANO KWA JINA VIRUSI, NA WIZI WA MUZIKI KUPITIA MTANDAONI. YAANI '***VIRUSES, SPAM AND MUSIC PIRATES'***

KATIKA KIPINDI KILICHOTANGULIA , MJOMBA KILU ANAJIFUNZA MENGI TU KUHUSU MATUMIZI YA RUNUNU YAANI SIMU YA MKONONI.KADHALIKA ZAPCOM NA GEORGE WANAJIFUNZA HUDUMA MBALI MBALI ZA SIMU KATIKA JUHUDI ZA KUIMARISHA BIASHARA YAO NA PIA MKAHAWA WA KULA TU FOODS.LAKINI WANAFAHAMU KWAMBA BADO WANASAFARI NDEFU YA KUJIFUNZA MENGI KUHUSU TEKNOLOJIA HII MPYA YA MAWASILIANO. HIVYO NATUMAI UTAENDELEA KUWA NASI HADI MWISHO USIKIE NI YAPI WANAYOENDELEA KUJIFUNZA. …

3. **A-SFX: A BUZZ OF EXCITEMENT. YOUTHFUL VOICES AND A BACKGROUND OF POP MUSIC AT A DISTANCE.**

4. **UNCLE KILU** **(SOUNDING HARRASSED AND SHOUTING ACROSS)**…George, George, njoo hapa upesi usaidie…umuhudumie yule mteja pale.

**5. GEOREG** Subiri dakika chache tu mjomba. Dakika moja tu…!

**6. B-SFX: BACKGROUND MUSIC AND EXCITEMENT INCREASES.**

**7. UNCLE KILU** (**GETTING ANGRY**) George, Nakuita hapa njoo haraka !

**8. C-SFX: MUSIC AND EXCITEMENT INCREASES.**

**9. UNCLE KILU** (**MUTTERING TO HIMSELF SOFTLY**) Unafanya nini? George nini kinachokugandisha hapo!. (**APPROACHES**).

**10. D-SFX: MUSIC AND EXCITEMENT GETS LOUDER AS HE APPROACHES**

**11. UNCLE KILU** (**TO OMWA**) Omwa, Kunaendelea nini hapa? Hamtaki kunijibu?. Umezipata wapi fedha hizi zote?

**12. OMWA** (**EXCITED**) Siku hizi pato letu limeongezeka sana Mzee. Wateja wananunua kwa wingi kanda hizi za CD pia!

**13. UNCLE KILU** (**PUZZED**) Eti CD?

**14.** **OMWA** (**STILL EXCITED**) Ehh ndio CD…! hizi kanda za muziki….! wamekuwa wakiunga foleni hapa mchana kutwa kununua hizi CD.

**15.** **UNCLE KILU** Muziki wa nani?

**16.** **OMWA** Wanamuziki wote, bora tu ni muziki maarufu unaopendwa na ambao tunaweza kuupata rahisi kwa mtandao wa Intaneti.

**17.** **UNCLE KILU** Sasa mnanikoroga akili. Mnarekodi muziki wa watu kutoka mtandaoni kwenye CD hizi na kuuuza?

**18.** **OMWA** Ndio! Njia rahisi sana ya kutengeneza pesa!. Sasa muda wangu umeisha nataka kwenda….. nahitaji kurekodi CD hizi!.

**19.** **ANNOUNCER** Mjomba Kilu amechanganyikiwa, haelewi ni nini kinachoendelea, namna muziki huo unavyorekodiwa kutoka mtandao wa Intaneti, au hata teknolojia inayotumika kurekodi muziki kutoka mtandaoni hadi katika kanda za CD. Na sasa ameamua kumtafuta ZAPCOM, mtaalam wake ili aweze kumfafanulia zaidi.

**SCENE TWO: KULA TU FOODS. LATE IN THE DAY.**

| | | |
|---|---|---|
| **20.** | **UNCLE KILU** | Zapu…mwanangu! hebu niambie kuhusu ule muziki unaouzwa na George na Omwa…! |
| **21.** | **ZAPCOM** | Una nini ? |
| **22.** | **UNCLE KILU** | Wameununua au vipi? |
| **23.** | **ZAPCOM** | Oh, ndio… wanatengeneza pesa nyingi sana kutokana na muziki huo...! |
| **24.** | **UNCLE KILU** | Hapana .. sio wao…! sio kuhusu biashara yako, nauliza muziki wanaouuza, wameununua kutoka kwa wanamuziki wenyewe au ni vipi….?… Wameuziwa…? |
| **25.** | **ZAPCOM** | (**LAUGHS**) Hapana mjomba, muziki huo ni bure, unapatikana bila malipo katika mtandao wa Intaneti. … Kuna tovuti mbalimbali kwenye mtandao ambako muziki unauzwa! Unachohitajika kufanya ni kutuma pesa tu na unapewa idhini ya kufungua muziki wao kupitia mtandao..! |

| | | |
|---|---|---|
| **26.** | **UNCLE KILU** | Sikuelewi..! Yaani wanawauzia na kisha bado unasema ni bure. Una maana kwa mfano mimi nitangaze biashara yangu ya supu kwa bei fulani kisha mwishowe watu waje kuinywa bure!. Inawezekanaje wanamuziki hao watoe muziki wao bure tu? |
| **27.** | **ZAPCOM** | **(A CONSPIRATORY WHISPER)** Kunazo njia nyingi za kufungua tovuti za muziki bila malipo katika mtandao wa Intaneti. |
| **28.** | **UNCLE KILU** | (**ANGRY**) Wezi nyinyi ! |
| **29.** | **ZAPCOM** | (**SURPRISED**) Eti nini? Usituite wezi!. |
| **30.** | **UNCLE KILU** | **(VERY ANGRY)** Basi nieleze, kama huo si wizi ni nini? Na zaidi mnaiba muziki huo na kisha kuuzwa! Je mnawalipa wenyewe sehemu ya pato linalotokana na biashara hii? Heeee ….nijibu!.. Hiyo ni haki kweli? |
| **31.** | **ZAPCOM** | (**UNCOMFORTABLE**) Sawa…ehh… lakini huo si wizi….. |
| **32.** | **UNCLE KILU** | (**FIRMLY**) Kama si wizi ni nini?. Sitaki tabia hii. Sitaki kuwa na washirika wa kibiashara ambao ni wezi. |

**33. ANNOUNCER** Kama si wizi ni nini?. Kuvuna mahali ambapo hujapanda!. Kunasa muziki mtandaoni bila ya idhini na kisha kuuza …ni hatia….. Ni wizi..!– Kwa Mjomba Kilu huo ni wizi hadharani !. Na amezua hoja za kimaadili na pia kisheria.. Hoja kwamba tunapasa kuwajibika na kufanya maamuzi ya busara kwa kuzingatia sheria zilizoko!

**MUSIC: BRIDGE MUSIC**

**SCENE THREE: AT THE INTERNET CAFÉ**

**33a OMWA** (**FRUSTRATED**) Zapcom, mara nyingine kazi yangu huwa ngumu sana katika mgahawa huu. Sielewi kabisa…. sijui nifanye nini….! Stakabadhi zangu zinapotea…. Na komputa hizi zimekataa kufunguka. Kwani kuna tatizo gani?

**34. E-SFX: DOOR OPENS. COUGHS, SNIFF, NOSE BLOWING. CHORUSES FILL THE AIR.**

**35. UNCLE KILU** (SURPRISED) Nini kinachoendelea hapa?.Kwani nimeingia katika wodi ya wagonjwa?

| | | |
|---|---|---|
| **35a** | **ZAPCOM** | (SNEEZING AND SPLUTTERING) Ni huyu George, ameleta virusi hapa! (TO OMWA) Omwa, Tafadhali nisaidie kufunga hizo komputa! |
| **36.** | **OMWA** | **(COUGHS)** Ooh hebu ngoja kidogo ....Kuna matatizo hapa....Hii komputa haitaweza kufunga vizuri!. |
| **37.** | **ZAPCOM** | Kwa nini?... (**PAUSE, SNEEZE**)... Oh hata hii pia! |
| **38.** | **OMWA** | Pia hii ina matatizo! |
| **39.** | **UNCLE KILU** | Kwani komputa zimefanywa nini? |
| **40.** | **ZAPCOM** | Ni komputa zote. Nafikiri zimeambukizwa Virusi! |
| **41.** | **UNCLE KILU** | Najua.... hii ndio sababu sisi zote tumeambukizwa homa na kuanza kutema tema kila mahali katika mkahawa huu! |
| **42.** | **OMWA** | Sasa huu ni mkasa...! (**COUGH**) Sasa tutafanya nini?. |
| 43. | UNCLE KILU | Suluhisho ni kwenda hospitalini. Ndio sababu zimejengwa eti..! Eeeee, zilijengwa kwa wagonjwa na hata wewe pia…..! |
| **44.** | **ZAPCOM** | Ni virusi ...! tunapasa .......... |

**45. UNCLE KILU** **(INTERRUPTS)** Basi tuache kuongea sana twendeni hospitalini.

**46. ZAPCOM** **(IRRITABLE)** Nazungumzia hizi komputa, zimeambukizwa virusi!.

**47. OMWA** (**SNIFF SNIFF**) Huu sasa ni mkasa!. Tutafanya nini sasa?

**48. UNCLE KILU** Mimi sijui. Wewe pia umeambukizwa homa na hizi komputa zenye virusi?

**49. ZAPCOM** Ni …ni…(**SNEEZE)** … ni kweli hizi Komputa zimeambukizwa virusi.

**50. UNCLE KILU** Hebu tueleze kijana, nafikiri virusi hivyo pia vimeathiri ubongo wako.

**51. ZAPCOM** (**COUGH**) Ni kweli mjomba. Virusi vilivyovamia komputa sasa vimezaana na kusambaa kwa haraka sana katika faili. (**SNEEZE**)

**52. UNCLE KILU** (**NOT EXACTLY UNDERSTANDING**) Basi hiyo ni hatari. Je kuna hospitali za kutibu komputa zenu?

**53. ZAPCOM** La ..tunachohitaji ni programu inayoweza kupigana vita na virusi hivi…sawa..! hebu nifafanue zaidi. Programu hizi za kupambana na virusi, ni kifaa kinachojulikana kama ***software*** ambacho kimetengenezwa hususan kupambana na virusi hivyo punde tu vinapovamia komputa.

**54. OMWA** **(SOUNDING VERY MISERABLE**) Kwa nini hamukuweka progamu hii mapema?

**55. ZAPCOM** Tuliweka, lakini kila mara aina mpya ya virusi hujitokeza na kuvamia komputa. Wakati aina mpya ya virusi inapojitokeza, kinga iliyoko kwenye komputa mara nyingine hushindwa kupambana kikamilifu na virusi hivyo, na hivyo unahitaji kuweka aina nyingine ya kinga kutibu virusi hivyo.

**56. OMWA** Sasa tufanyeje? Siwezi kukaa tu bila kazi yoyote ya kufanya!

***57.*** **ZAPCOM** Nitahakikisha kwamba, mbali na kuweka aina mpya ya kinga, pia tuna programu nyingine inayojulikana kama ***Firewall.***

**58. UNCLE KILU** ***Fire wall*** ni nini?

**59. ZAPCOM** ***Firewall*** ni programu inayowekwa kwenye Komputa kuchunguza mawasiliano yote yanayoingia na kutoka kwenye Komputa. Pia programu hii huzuia baadhi ya mawasiliano chini ya sheria fulani zilizowekwa. Ni kama mlinzi anayewazuia au kuruhusu wageni kuingia nyumbani kwako.

**60. UNCLE KILU** Teknolojia hiyo ni ngumu kuielewa.

**61. ZAPCOM** Si lazima, lakini chukulia tu mfano wa kichungi. Kichungi unachotumia jikoni. Kazi yake ni kuchuja uchafu ambao huuhitaji. Kichungi hicho ni sawa na Programu ya ***Fire Wall*** kwenye Komputa yako. (**SNIFFLES**)

**62. UNCLE KILU** Kumbe…..!

**63. OMWA** Sasa tunasubiri nini? Twendeni tutafute hiyo Programu ya ***Fire Wall*** na kinga ya virusi haraka. (**COUGHS**)

**64. F-SFX: MORE UNCONTROLABLE SNEEZING, COUGHING AND NOSE BLOWING**

**65. OMWA** Hii ni shida. Pia Komputa zimejaa barua zisizo na maana kwenye anwani zetu za e-mail.

**66. ZAPCOM** Ndio, sasa hiyo inayojulikana kwa lugha ya kisayansi kama ***spam mail***. Tunapaswa pia kuzitambua na kuzitupa katika kijisanduki maalum cha taka kwenye komputa kinachojulikana kama ***Junk folder***.

**67. OMWA** Watu hawa wanaotuma barua hizi wanapaswa kushtakiwa. Hawapaswi kutatiza kazi zetu kwa kutengeneza na kututumia virusi kila mara.

**68. ZAPCOM** (**TO OMWA**)…Ama kwa hakika ulimwengu umekuonea Omwa. Baadhi ya virusi hivi hupitia mtandao wa Intaneti na vingine hubebwa kwenye vifaa maalum vya kuhifadhi habari vinavyojulikana kama ***Flash disks*** ambavyo hutumiwa sana na wateja wetu hapa. Nani ajuaye, labda hao wateja ndio wanaoleta virusi hivi? (**SNEEZES**)

**69. OMWA** Sasa twendeni hospitalini. Tayari yamemwagika hakuna haja ya kumlaumu sana George. (**SNIFFLES)**

**MUSIC: BRIDGE MUSIC**

**70. ANNOUNCER** Kwa mara nyingine kundi la vijana linaendelea kujifunza mengi kwamba teknolojia inayowaunganisha na ulimwengu mzima, ndiyo hiyo hiyo inayowaletea mambo mengine yasiyohitajika. Wanahitajika kuwa waangalifu kila wanapotumia mtandao wa Intaneti. Licha kwamba mtandao hutoa habari muhimu kwa jamii nzima, kuna wale ambao juhudi zao zinaelekezwa katika kuvuruga na kufanya maisha ya wengine kuwa magumu.

**71. ANNOUNCER** Kundi hili la vijana pia linajifunza kuwa ni lazima liwe makini katika biashara yao ya huduma za Intaneti. Kila unapounganishwa na huduma hizi na kadhalika wengine kutumia Komputa yako, kuna hatari ya kusambaziwa virusi vya aina mbalimbai. Je, komputa zao zitafufuka. Na je wataendelea kufungua kurasa na kunasa miziki katika kanda za CD kinyume na sheria? Ni yapi yatakayotokea baadaye?

Ungana nasi kwa makala yajayo tunapoendelea kufutalia mchezo huu. Tembembelea tovuti yetu www.dw-world.de/Ibe Hadi wakati huo basi Kwaheri kwa sasa.